Ubatito wa Yesu

na

Ellis P. Forsman

(The Baptism of Jesus)

Ubatizo wa Yesu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 14, 2011

Ubatizo wa Yesu

Mat. 3:13-17

Mat. 3:13-17, "*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Jordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*"

Yesu alipobatizwa na Yohana kulionyesha umuhimu mkubwa katika huduma yao…

Ilikuja wakati muhimu wa huduma ya Yohana ambayo mara alianza kukataa.

Ilifanyika kama mwanzo wa huduma wa Yesu, ambayo mara ilichukua nafasi ya huduma ya Yohana.

Kiuhalisia ubatizo wa Yesu huibua baadhi ya maswali… Kwa nini alibatizwa?

Je inaonyesha maelezo ya kusudi la ubatizo wa Mkristo?

Katika somo hili tutajaribu kujibu maswali haya, kwanza kwa kuangalia historia kuhusu ubatizo wa Yesu.

Ubatizo wa Yesu

Yesu anakuja kwa Yohana

Kutoka Galilaya mpaka mto Yordani.

Mat. 3:13, "*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Jordani kwa Yohana ili abatizwe.*"

Yesu alikuwa akiishi Nazareti, mji wa Galilaya.

Mat. 2:23, "*Akaenda akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii, Ataitwaa Mnazorayo.*"

Yohana alikuwa akibatiza katika mto Yordani, palipokuwa na maji tele.

- Mat. 3:5-6, "*Ndipo walipomwendea Yerusalemu, na Uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya Jordani; naye akawabatiza katika mto wa Yordani, huku wakiziungama dhambi zao.*"
- Yoh.3:23, "*Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea wakabatizwa.*"

Yesu alimwendea Yohana ili ambatize.

Mat. 3:13, "*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe.*"

Yohana anatafuta kumzuia Yesu.

Yohana alijaribu kumzuia Yesu ili asimbatize.

Mat. 3:14, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?*"

Yohana anaeleza ni kwa nini: "Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?

Kuna hali fulani ya mshituko katika maneno ya Yohana. Yohana alijua kwamba Yesu ni mtu wa Mungu, labda kwa sababu ya maneno yake na uelewa, lakini hakujua kwamba Yesu alikuwa Masihi hadi pale aalipombatiza. Bila shaka, alipokaribiwa na Yesu, kidogo alimshukia.

Matukio katika kifungu kifuatacho yalitokea siku moja baada ya kumbatiza Yesu.

Yoh. 1:29-33, "*Siku pili yake amwona Yesu anakuja kwake akasema tazama Mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. <u>Wala mimi sikumjua; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli</u> ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji. Tena Yohana akashuhudia akisema, nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake. <u>Wala mimi sikumjua</u>; lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu.*"

Yesu anamsshawishi Yohana.

Yesu anamshawishi Yohana aruhusu ubatizo wake.

Mat. 3:15, "*Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali.*"

Yesu anaeleza ni kwa nini: "*...kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote…*" (Zaidi kuhusu hili baadaye).

Hivyo, Yesu anabatizwa na Yohana.

Roho na Baba wanaongeza ushuhuda wao:

Mat. 3:16, "*Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake.*"

Mbingu zikamfunukia, na Roho wa Mungu akashuka kama hua (katika hali ya kiwiliwili, Luka 3:22) na mianga juu ya Yesu.

Luka 3:22, "*Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua; sauti ikatoka mbinguni, wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe.*"

Sauti kutoka mbinguni inatangaza:

"*Huyu ni Mwanangu.*"

"*Ninayependezwa naye.*"

Hii ndiyo mara ya kwanza Mungu anamkiri Yessu kwa sauti kama Mwana wake. Tunafanyika wana wa Mungu tunapobatizwa.

Pasipo swali, ubatizo wa Yesu lilikuwa ni tukio muhimu! Kiuhalisia inaibua maswali kadhaa ambayo nitajaribu kujibu…

Maswali yanayohusiana na ubatizo wa Yesu:

Kwa nini Yesu alibatizwa?

Kwa uwazi, siyo kwa sababu ileile iliyofanya watu wengine wabatizwe na Yohana. Ubatizo wao ulikuwa wa toba kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

Mk.1: 4, "*Yohana alitokea akibatiza nyikani, na kuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi*."

Walikuwa wanakiri dhambi zao.

Mk. 1:5, "*Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto Yordani wakiziungama dhambi zao.*"

Mat. 3:6, "*Naye akawabatiza katika mto wa Yordani, huku wakiziungama dhambi zao.*"

Lakini, Yesu hakuwa na dhambi.

Heb. 4:15, "*Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.*"

Sasa, kwa nini Yesu alibatizwa? Yesu alisema "*ilikuwa ni kutimiza haki yote.*" (Mat. 3:15).

Ilikuwa ni shauri la Mungu kwamba watu wabatizwe na Yohana.

Luka 7:29-30, "*Na watu wote na watoza ushuru waaliposikia hayo waliikiri haki ya Mungu, kwa kuwa wamebatizwa kwa ubatizo wa Yohana. Lakini Mafarisayo na wanasheria walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye.*"

Yesu angesema, “Kwa nini nibatizwe? Wakati sina dhambi!”

Yesu alitaka kuweka mfano sahihi kwa kufanya mapenzi ya Baba, kitu alichopenda kufanya.

- Zab. 40:7-8, “*Ndipo niliposema tazamaa nimekuja, katika gombo la chuo nimeandikiwa, kuyafanya mapenzi yako, ee Mungu wangu ndiyo furaha yangu; naam sheria yako imo moyoni mwangu.*”
- Yoh. 4:34, “*Yesu aakawaambia chakula change ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake.*”
- Yoh. 8:29, “*Naye aliyenipeleka yu pamoja nami, hakuniacha pekee yangu; kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo.*”

Yesu alibatizwa kwa sababu ni kitu ambacho Baba yake alitaka akifanye.

Ilifanyika hivyo ili kumtambulisha Yesu kwa Yohana na Israeli.

Yohana alikuwa akitangaza kwamba Masihi anakuja.

Mat. 3:11, “*Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatizaa kwa Roho Mtakatifu na kwa moto.*”

Yohana aliambiwa kwamba Roho kuja juu ya mtu ilikuwa ni ishara kwamba yeye ni Masihi, Mwana wa Mungu.

Yoh. 1:29-34, “*Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake aakasema, tazama Mwana-kondo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba yuaja nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. Wala mimi sikumjua ; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji. Tena Yohana ashuhudia akisema, nimemwona Roho akishukaa kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake. Wala mimi sikumjua; lakini yeye aliyenipelekaa kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu. Nami nimeona, <u>tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu</u>.*”

Je ubatizo wa Yesu unaelezea kusudi la ubatizo wa Mkristo?

Wengi wanachukulia ubatizo wa Yesu ili watafsiri vibaya ubatizo wa Wakristo.

Kwamba ubatizo wetu hauhusiani na ondoleo la dhambi. Kwa ubatizo wetu ni kuonyesha imani yake mbele ya halaiki.

Kwamba ubatizo wetu ni uwazi wa kutambua uhusiano wetu na Kristo, kama ambavyo ubatizo wake ulimtambulisha kwa Israeli.

Hata ivyo, hakuna muunganiko wowote wa kibiblia uliofaanywa kati ya ubatizo wa Yesu na wetu wenyewe.

Ubatizo wa Mkristo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Anania alimwambia Sauli (Paulo), Mdo. 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukilitia jina lake.*"

Ubatizo wa Mkristo ni muunganiko na Kristo katika mauti yake.

Rum. 6:3-7, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye kaatika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena; kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi.*"

Hakuna mwandishi wa Biblia aliyewahi kuandika kwamba tunabatizwa kwa sababu inayofanana na ule wa Yesu.

Kuna umuhimu gani wa Roho kushuka na sauti ya Baba?

Kimsingi yanashuhudia kwamba Yesu ni nani.

Kama ambavyo Roho angefanya baadae, kwa kazi alizozifanya Yesu.

Mat. 12:28, "*Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia.*"

Kama ambavyo Baba angefanya baadae, katika tukio lingine.

Mat. 17:5, "*Alipokuwa katika kusema, tazama wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama sauti ikatoka katika lile wingu ikasema, huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.*"

Mungu alisema haya baada ya Petro kudhani ana mawazo mazuri ya kujenga mahema matatu; moja ya Musa, moja ya Elia, na moja kwa ajili ya Yesu.

Wao pia hutoa ushahidi katika asili ya uhusiano na mamlaka ya Mungu, Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu.

Hitimisho

Kwa ubatizo wa Yesu…

Hapo mwanzo alitambulishwa kwa Yohana, naye kwa Israeli.

Yoh. 1:29-34, "*Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake aakasema, tazama Mwana-kondo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba yuaja nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. Wala mimi sikumjua ; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji. Tena Yohana ashuhudia akisema, nimemwona Roho akishukaa kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake. Wala mimi sikumjua; lakini yeye aliyenipelekaa kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu. Nami nimeona, <u>tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu</u>.*"

Baba na Roho walimthibitisha kwa kunena na kuona kama Mwana.

Yesu alionyesha nia yake katika "*kutimiza haki yote*".

Kimsingi ubatizo wa Yesu inaumuhimu kwa Wakristo. Sio kwamba tulibatizwa kwa sababu inayofanana na ile ya Yesu. Bali kimsingi ni kuthibitisha kwamba alikuwa Masihi.

Na kuonyesha mtazamo unaowezaa kuwa sahihi kwa wanafunzi wake: "*Nimekuja kufanya mapenzi ya Baba.*"

Yesu <u>hakuhitaji</u> ubatizo, kwa sababu hakuwa na dhaambi; lakini hataivyo alibatizwa kwa sababu yalikuwa ni mapenzi ya Baba kwa wanadamu wote.

Je sisi wenye dhambi tunaweza kusita kufanya mapenzi ya Baba kuhusiana na ubatizo leo?

- Mat. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi endeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; <u>na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi</u>; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.*"
- Mk. 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. <u>Aaminiye na kubatizwa ataokoka</u> asiyeamini, atahukumiwa.*
- Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, <u>tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu</u>, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"